**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,**
Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma kwa kutujaalia uzima na Afya njema tukaweza kukutana tena katika Baraza hili la Kumi kwa ajili ya kuendelea kuwatumikia wananchi wetu.

**Mheshimiwa Spika,**
Nichukue fursa hii kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii adhimu na muhimu ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,**
Vile vile, napenda kuchukua nafasi kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan pamoja Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kufanikisha kupatikana na kutengwa fedha za Uviko 19 kwa ajili ya Sekta muhimu ya Afya.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati yetu inatoa pongezi za dhati kwa Waziri wa Afya Mheshimiwa Nassor Ahmed Mazrui pamoja naNaibu Waziri wa Afya Mheshimiwa Hassan Khamis Hafidh kwa umahiri na umakini wao wa hali ya juu waliouonesha kila wakati Kamati ilipokutana na Wizara hii. Shukurani za kipekee tunazitoa kwao kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia katika kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Vile vile, tunatoa shukrani za dhati kwa Katibu Mkuu Ndugu. Dkt. Fatma H. Mrisho na watendaji wote wa Wizara hii kwa ushirikiano waliotupatia katika utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Kamati hususan katika kupitia Bajeti ya Wizara ya Afya.

**Mheshimiwa Spika,**
Sambamba na hilo, Shukurani za pekee nazitoa kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa ujasiri wao waliouonesha katika kujadili Makadirio ya Mapato

na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2022/2023 na hatimae kuipitisha bajeti Wizara hii. Kwa heshima kubwa napenda kuwatambulisha Wajumbe hao kwa majina kama hivi ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mheshimiwa Mohamed Ahmada Salum | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis | - | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mheshimiwa Abdalla Abasi Wadi | - | Mjumbe |
| 4. | Mheshimiwa Bihindi Hamad Khamis | - | Mjumbe |
| 5. | Mheshimiwa Haji Omar Kheri | - | Mjumbe |
| 6. | Mheshimiwa Zawadi Amur Nassor | - | Mjumbe |
| 7. | Ndg. Fatma Omar Ali | - | Katibu |
| 8. | Ndugu Mussa Issa Mussa | - | Katibu |
| 9. | Ndugu Azmina Hamad Khamis | - | Msaidizi |

**Mheshimiwa Spika,**
Jadweli la kwanza ambalo limeundwa chini ya Kanuni ya 107(3)(v)ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020), inazitaka Kamati za kisekta kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Wizara husika ya Mapato na Matumizi ya kila mwaka. Katika utekelezaji wa matakwa ya Kanuni hiyo, Kamati ya Ustawi wa Jamii ilitekeleza wajibu wake kwa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya mnano tarehe 20/04/2022 kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,**
Baada ya Maelezo hayo, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati ya Ustawi ya Jamii naomba niwasilishe mbele ya Baraza Lako Tukufu Maoni ya Kamati yangu kuhusiana na Bajeti hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**
Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha **2022/2023** ina Mafungu (votes) **mbili (2),FunguH01 Wizara ya Afya** na imepanga kutekeleza Programu Kuu Tatu(3) zenye Programu Ndogo Saba **(7)**na **Fungu HO2 Hospitali ya Mnazi Mmoja** na imepanga

kutekeleza Programu Kuu Mbili (2) zenye Programu Ndogo Tatu (3) na ambapo kwa ujumla fedha zilizoombwa kwa Wizara ya Afya **TZS. 188,213, 458, 000/= (Bilioni Mia Thamanini na Nane, Milioni Mia Mbili na Kumi na Tatu,Laki Nne na Hamsini na Nane**.

## FUNGU H01 WIZARA YA AFYA

## PROGRAMU KUU YA HUDUMA ZA TIBA

**Mheshimiwa Spika,**
Utekelezaji wa Programu hii unatekelezwa kupitia Programu Ndogo mbili (2), isipokuwa Kamati itajikita zaidi katika **Programu Ndogo ya Huduma za Matibabu (SH010201)** na kuzungumzia katika **Huduma ya HH01020101** inayohusiana na Huduma za Hospitali za Vijiji, Wilaya na Hospitali za Rufaa.

**Mheshimiwa Spika,**
Tunachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuimarisha Sekta ya Afya kwa kujenga Vituo vya Afya pamoja na kuhakikisha huduma za afya zinaimarika nchini.

Hata hivyo, Kamati imebaini bado kuna haja ya Zahanati zetu za Vijijini pamoja na Hospitali za Wilaya na Rufaa kuhakikisha vinapatikana vifaa tiba pamoja na wafanyakazi wa kutosha ikiwemo wataalamu waliobobea katika kada tofauti za Utabibu, ili huduma hizi ziendelee kupatikana katika maeneo ya karibu  na wananchi kama lengo la Serikali lilivyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,**
Wakati Kamati ilipokuwa ikifanya kazi zake za ufuatiliaji wa bajeti kwa wizara hii ilibahatika kutembelea baadhi ya hospitali zilizopo Unguja na Pemba na kubaini changamoto kadhaa ikiwemo ya upungufuvifaa muhimu kwa baadhi ya hospitali kama vile X-ray, CT Scan, MRI, Full Blood Picture, Ultra Sound, hali hiyo inapelekea huduma hizi kukosekana kwa  wananchi wanaofika katika hospitali hizo kwa ajili ya kufuata huduma hizo.

**Mheshimiwa Spika,**
Aidha, Kamati imegundua hasa Hospitali ya Wilaya Makunduchi, Hospitali ya Mkoa ya Abdalla Mzee Hospitali Mkoani kwambakuna vifaa vya kisasa ambavyo havitumiki kutokana na watendaji hawana ujuzi wa matumizi ya vifaa hivyo na kupelekea kuharibika bila ya kutumika, jambo ambalo ni upotevu wa rasilimali fedha za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,**
Kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri Serikali pale inaponunua vifaa kwa ajili ya matumizi ya Sekta ya Afya, kabla vifaa hivyo kukabidhiwa kwa wahusika ni muhimu kwanza kutolewa kwa elimu kwa watendaji juu ya matumizi ya vifaa hivyo, ili kuepusha uharibifu wa mara kwa mara au kukaa kwa muda mrefu bila ya kutumika.

**Mheshimiwa Spika,**
Vile vile, Kamati inashauri tena Serikali kupitia Wizara ya Afya kuandaa Mpango Mkakati kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuanzisha masomo ya Kada Adimu au muhimu kwa mahitaji ya nchi yetu ikiwemo Kada ya Mionzi, Kada ya Masomo ya Usingizi (Ganzi) pamoja na kada nyenginezo, kwa lengo la kupunguza changamoto yaukosefu wa wataalamu wazawa. Sambamba na hilo, tukizingatia ujenzi wa hospitali mpya za Wilaya na Mikoa unaoendelea.

**Mheshimiwa Spika,**
Hivyo, tukiweza kufanya hivyo tutakuwa na wataalamu wengi zaidi wazawa na wenye fani tofauti ndani ya nchi yetu na kuweza kuokoa fedha nyingi kwawananchi ambao hufuatia huduma nje ya nchi kwa kupatiwa matibabu hapa nchini kwetu bila ya kusafiri.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA AFYA

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati imebaini kuwa kuna Taasisi za Serikali ikiwemo Baraza la Tiba, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala, Taasisi ya Utafiti wa Afya, Bodi ya Madaktari zinazohusiana na Afya kuchukua juhudi kubwa ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali kupitia vyanzo vyao tofauti vya ndani, lakini bado wanakabiliwa na changamoto kwa sababu fedha zote zinazokusanywa na Taasisi hizo zinakwenda katika Mfuko Mkuu wa Hazina na wala hakuna chochote kinachorudi kwa Taasisi hizo, hali inayopelekea kushindwa kutekeleza majukumu yao ya msingi yaliopo kwa mujibu wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati, inapendekeza kwa Taasisi hizo ambazo zinakusanya mapato ziruhusiwe kutumia angalau sehemu ya makusanyo hayo kwa ajili ya uendeshaji wa majukumu katika Taasisi hizo, ili wawezekutimiza malengo yao waliyojiwekea na kuacha kutegemea ruzuku ama OC pekee. Kwa kweli Taasisi hizo nyingi haziko vizuri katika utekelezaji wa majukumu yao, kwa kutegemea ruzuku ama OC ambazo huwa hazipatikani kwa wakati na kinachopatikana huwa ni kiwango kidogo.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa upande wa Bodi ya Hospitali Binafsi, Kamati inaipongeza Bodi hiyo kwa utendaji kazi wake kwa kuweza kulipa kwa wakati asilimia mia moja kwa mwaka 2021/2022, kwa mnasaba huo Bodi haina. Kutokana na hali hiyo, Kamati inatoa wito kwa Taasisi nyengine ambazo zinatakiwa kulipa kuiga mfano huo mzuri wa Bodi hiyo, kwa kuweza kulipa vizuri na kwa wakati kwa lengo la kuchangia pato la Taifa.

## PROGRAMU NDOGO YA URATIBU WA MIPANGO, SERA NA TAFITI ZA WIZARA

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati, inapongeza juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Wizara ya Afya katika kutekeleza pamoja na kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Ujenzi wa Hospitali za Wilaya na Mikoa zinazotekelezwa kutokana na fedha za Ahuweni ya Uviko 19. Licha ya changamoto mbali mbali wanazokumbana nazo katika utekelezaji wa miradi hiyo, Wizara ya Afya haikusita kuunda Timu Maalum ya Wataalamu pamoja na kuweka Washauri Elekezi wa miradi hiyo kwa Unguja na Pemba, ili kuona miradi hiyo inayojengwa itakapokamilika iwe katika viwango pamoja na ubora unaostahiki.

**Mheshimiwa Spika,**
Pia tunachukua nafasi hii kuipongeza Timu ya Maalum Wataalamu ya ufuatiliaji wa miradi hii pamoja na Washauri  Elekezi kwa kufanya kazi kwa uzalendo wao bila ya kujali maslahi binafsi isipokuwa kuweka maslahi mapana ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,**
Aidha, matarajio ya Kamati ni kwamba baada ya kukamilika kwa ujenzi wa Hospitali hizo kutapunguza msongamano kwa wagonjwa wanaofika katika Vituo pamoja na Hospitali zetu kwani kila Wilaya na Mikoa itakuwa na Vituo vyake vya Afya pamoja na Hospitali zake. Sambamba na hilo, Kamati inatoa wito kwa wananchi wakati utakapofika kuzitumia Hospitali zetu za Wilaya na Mikoa kwa ajili ya kupata huduma za matibabu kufanya hivyo na kuacha kukimbilia Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja, ili kuondosha usufumbufu na msongamano katika hospitali hiyo.

## FUNGU H02 HOSPITALI YA MNAZI MMOJA

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati, imebaini utaratibu wa uingizwaji wa fedha za bajeti kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja, fedha ambayo inayoingizwa kwa kila kwa mwaka ni tofauti na kiwango kilichoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi katika Bajeti ya mwaka 2021/2022. Aidha, hali hiyo imepelekea baadhi ya huduma au majukumu kutekelezwa chini ya kiwango na nyengine kukosekana kabisa. Mfano halisi kwa upande wa Dawa kwa Fungu H02 Hospitali ya Mnazi Mmoja fedha zilizoidhinishwa zilikuwa ni shilingi bilioni 35.6, lakini fedha zilizopatikana ni shilingi bilioni 30, hali iliyopelekea Hospitali ya Mnazi Mmoja kukabiliwa na changamoto ya madeni ya waletaji wa dawa (suppliers).

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati, inaishauri Serikali kupitia bajeti ya mwaka 2022/2023 kuliongezea bajeti Fungu H02 la Hospitali ya Mnazi Mmoja, ili kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi ya kuwahudumia wananchi au wagonjwa wanaotoka Hospitali mbali mbali za Unguja na Pemba na kuweza kutekeleza kwa vitendo dhana ya Hospitali ya Rufaa.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa kumalizia Kamati inatoa wito kwa watendaji pamoja na wataalamu wa Sekta ya Afya wafanye kazi kwa bidii na maarifa, wazidishe uzalendo na kuwa wastahamilivu

licha ya changamoto zinazowakabili. Ni imani yetu kwamba Serikali inazifahamu changamoto zao na inazifanyia kazi kwa ajili ya kuzitatua ikiwemo masuala ya rasilimali watu, vifaa pamoja na maslahi, kwa lengo la kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi, Kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais wakati alipokuwa akizindua Mradi wa Kusafishia Maji ya Chumvi pamoja na Jengo la Kuhifadhia Maiti mnamo tarehe 12 Februari, 2022.

**Mheshimiwa Spika,**
Mwisho kabisa, napenda kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili Tukufu kwa umakini na usikivu wao wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii. Kwa vile Kamati ya Ustawi wa Jamii imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya naomba sasa nichukue fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kuichangia, kuijadili, kuhoji na hatimae kuipitisha bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa Fedha wa 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,**
Baada ya kusema hayo, Kwa niaba Kamati ya Ustawi wa Jamii pamoja na wananchi wa Jimbo la Malindi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.
Naomba kuwasilisha.

Ahsante,



……………………..

**Mhe. Mohamed Ahmada Salum,**
**Mwenyekiti**
**Kamati ya Ustawi wa Jamii,**
**Baraza la Wawakilishi,**
**<u>Zanzibar.</u>**